



Mbuzi, Mbwa na Ng'ombe
walikuwa marafiki
wakubwa.

Siku moja walisafiri kwa
teksi.



Walifika mwisho wa safari
yao.

Dereva aliwauliza walipe
nauli zao.

Ng'ombe akalipa.



Mbwa hakuwa na kiasi
kamili cha pesa, akalipa
zaidi kidogo.



Dereva alikuwa
anajitayarisha
kumrudishia Mbwa baki ya
pesa zake.

Wakati huo, Mbuzi
alitoroka bila kulipa
chochote.



Dereva akakasirika sana.

Akaondosha gari bila
kumrudishia Mbwa baki ya
pesa zake.




Hiyo ndiyo sababu, siku zote, Mbwa hulikimbilia gari.

Nia yake ni kumpata dereva amrudishie baki ya pesa zake.



Mbuzi, anapousikia mlio
wa gari, hutoroka.

Yeye huogopa kushikwa
kwa kukosa kulipa nauki.



Ng'ombe huwa
hashughuliki gari
linapokuja.

Yeye huchukua muda
kuvuka barabara.

Anajua kwamba alilipa
nauli yake kamili!